

## **MKUU WA MKOA WA RUVUMA MHE. BINILITH MAHENGE ASHIRIKI WIKI YA USAFI NA MAZINGIRA WILAYANI NYASA.**

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Ndg. Binilith Mahenge ameshiriki Wiki ya kampeni ya Usafi na Mazingira Kimokoa Wilayani Nyasa kwa kufanya usafi kwenye Fukwe za ziwa Nyasa pamoja na wananchi wa Mji wa Mbamba bay tarehe 03-06-2017

Awali ya yote, Mh. Mkuu wa Mkoa aliwasili Wilayani Nyasa majira ya saa 08.30 na kupokelewa na Mkuu wa Wilaya ya Nyasa Mh. Isabela Chilumba na kuelekea moja kwa moja kwenye fukwe za ziwa zilizoko pembezoni mwa Mji wa Mbamba bay na kuanza kufanya usafi ambapo alikuta tayari Mkuu wa Wilaya ya Nyasa na Wananchi wanaendelea na kazi hiyo.

Baada ya zoezi hilo Mkuu wa Mkoa alisomewa Taarifa ya Wilaya ambayo ilijikita zaidi kuelezea ali alisi ya Usafi na Mazinira Wilayani Nyasa. Akisoma Taarifa iyo Kaimu Mkuruenzi wa halmashauri ya Wilaya ya Nyasa Eng.Evaristo Ngole alisema Hali ya Usafi katika mji wa mbamba bay ni nzuri wasitani na inaendelea kuimarika kutokana na uongozi wa Wilaya kuendelea kuhamasisha na kutoa elimu kwa njia ya Mikutano, Radio na vikao vya watumishi

Kwa sasa mji wa Mbamba bay hauna eneo la dampo kutokana na jografia ya mji kuzungukwa na milima na mito, jambo linalopelekea taka zinazozalishwa kutupwa kiholela hususani kando ya barabara inayoenda kilosa.

Hata hivyo wilaya imepata eneo linalofaa kwa dampo ambalo lipo katika kijiji cha Nangombo km 11 kutoka mji wa Mbamba bay ambalo linahitaji kulipwa fidia ndipo lianze kutumika.

Aidha wilaya inaendelea kuhimiza watu kuchimba mashimo kwa ajili ya kutupa takataka na kuchoma moto pindi tunaposubiri ujenzi wa viguba na dampo. Hatua hii kwa sasa imeonekana ndiyo jibu sahihi la kukabiriana na utupaji wa taka kiholela.

Aidha Eng Ngole alimweleza Mh. Mkuu wa Mkoa kwamba Wilaya imeendelea kutekeleza agizo la kufanya usafi kila mwisho wa mwezi hususani katika maeneo ya umma ambapo zoezi hili limekuwa likitekelezwa katika ngazi zote kuanzia kitongoji, kijiji hadi kata.

Idara ya afya na mazingira imeendelea kuhamasisha jamii juu ya umuhimu wa kufanya usafi katika maeneo yao na maeneo yanayomilikiwa na umma na kwamba zoezi hili linafanyika kila jumamosi.

Akizungumza baada ya kusomewa taarifa hiyo, Mkuu wa Mkoa aliushukuru Uongozi wa Wilaya na Wananchi waliojitokeza kushiriki nae zoezi hilo maalum na kwamba anaendelea kuwatia moyo ili zoezi hilo liendeleo kuwa Muhimu kwa kuwa linahusu pia maisha yao, Aidha ameagiza mambo yafuatayo kwa uongozi na wananchi wa Nyasa

1. Kuendelea na zoezi la kufanya usafi kila jumamosi ya Mwisho wa mwezi na ikiwezekana kila jumamosi
2. Kuendelea na tabia ya upandaji Miti ambapo Nyasa imebarikiwa sana kwa kuwa Miti yenye thamani kubwa inapandwa na kustawi kwenye hali ya hewa ya eneo hili
3. Usafi wa Fukwe na maeneo mengine ya Nyasa yataongeza uwezekano wa kuongeza utalii wa ndani na nje kwa kuwa hakuna mtalii anayeweza kutembelea sehemu chafu ili kuifanya Nyasa kuwa Kitovu cha utalii kusini mwa Tanzania.
4. Shughuli ya usafi na mazingira isihusishwe na siasa hata kidogo
5. Halmashauri ya Wilaya ya nyasa itenge fedha kwenye bajeti zake kwa ajili ya Kujenga dambo na kununua vitendea kazi kama Magari na vingine kwa kuwa mji wa Mbamba bay unaotarajiwa kuwa wa Kitalii unakua kwa kiasi kikubwa.
6. Ameupongeza uongozi wa Wilaya kwa kuanzisha kikundi cha Uhamasishaji usafi na kuahidi kuwapa wanakikundi fedha jumla ya tsh. 1,000,000

Mwisho Mkuu wa Mkoa alitembelea eneo ambalo patafanyika uwekezaji kwa kujenga fish house itakayotumika kwa ajili ya maonyesho ya Samaki wa Mapambo wanaopatikana katika ziwa Nyasa